


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI

03 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA ISHIRINI – TAREHE 03 MEI, 2019

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

158. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mafuriko yaliyotokea Mlalo mwaka 1993 yalisababisha uharibifu mkubwa kwa barabara inayounganisha Tarafa za Umba na Mtae:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kukarabati barabara hiyo muhimu.

159. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Barabara ya Segerea Sheli kwenda Kipawa kuitia Seminari itaanza kutengenezwa.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

160. MHESHIMIWA HAMADI SALIM MAALIM (KOJANI)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:- Uvubi ni moja ya Vipaumbele vinavyosaidia kusukuma maendeleo ya Wananchi wengi wa Tanzania na Taifa letu ni mionganini mwa Mataifa maskini Duniani:-

Je, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga namna gani katika kuwasaidia Wavubi wadogo ili kukuza maendeleo ya Taifa pamoja na kujikwamua na umaskini uliokithiri

161. MHESHIMIWA MBARAKA KITWANA DAU (MAFIA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana mpaka sasa kwenye Tozo (*entrance fee*) ya kuingia maeneo ya Hifadhi ya Bahari (*Marine Park*) katika Kisiwa cha Mafia.

WIZARA YA MAJI:

162. MHESHIMIWA GIMBI DOTTO MASABA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Serikali iliahidi kujenga mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kuanzia Nyashimo, Ngasamo, Dutwa, Bariadi, Itilima, Meatu na Maswa:-

Je, ni lini mradi huo utaanza na kukamilika.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

163. MHESHIMIWA ALMAS ATHUMAN MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Waajiri wamekuwa wanalipa Tozo ya Maendeleo ya Ujuzi kwa Wafanyakazi (SDL) ya asilimia 4.5 ya mshahara kwa kila Mfanyakazi ambayo ililengwa kupelekwa VETA kwa lengo la kuendeleza ujuzi:-

(a) Je, ni asilimia ngapi ya Tozo hiyo inapelekwa VETA;

- (b) Je, ni lini Serikali itairejesha VETA katika Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuleta uwiano na mantiki kuwa VETA inaendeleza ujuzi kwa Wafanyakazi.

WIZARA YA KILIMO:

164. MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (RUFIJI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Bonde la Mto Rufiji lina eneo kubwa lenye rutuba ambalo lingetumika vizuri lingeweza kulisha Mji wa Dar es Salaam na Viwanda vyote nchini, RUBADA imechukua maeneo hayo ambayo inakadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta 500,000 na kuwapa baadhi ya Wawekezaji ambao wengi wao ni matapeli na madalali wa viwanja/mashamba:-

Je, lini Serikali itaamua kunyang'anya maeneo yote ambayo Wawekezaji wameshindwa kuwekeza kwa kadri walivyoomba ili Sera ya Serikali ya Viwanda iweze kutimia.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**165. MHESHIMIWA AMINA NASSOR MAKILAGI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Baadhi ya watu katika jamii bado wanaendeleza vitendo vya kuwanyanyasa, kuwadhalilisha na kuwadhulumu Wanawake:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutokomeza kabisa vitendo hivyo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
03 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**